




## MAONO YALIYOFAFANUA UPENDO WA MUNGU

## MAONO YA KUSHANGAZA

WAKATI MUNGU MKUU MWENYEZI Aliniwasilishia *karatasi iliyoandikwa* na Mikono YAKE mwenyewe katika maono ya Mei tarehe11, mwaka wa 2009 usiku, ilifanyika wakati mwingine wa *elekeo nyororo ya Moyo* WAKE kwa kanisa la Kristo la siku hizi. Maono ya ajaabu namna hii yanatafsirikaA moja kwa moja kuwa *Upendo Usiokwisha* na *neema iliofunuliwa* kwa wanadamu. Haya maono ya kushangaza ya Karatasi Iliyoandikwa na Mkono wa MUNGU mwenyewe, yanatufunulia *ujumbe* wa kilindini uliodhihirika wakati Yesu Alijiwasilisha kama mtoto mdogo kwenye hori ya ng'ombe ya Bethlehemu, na kama Mwokozi Aliyewaponya wagonjwa na kufufua wafu na kupaka *marhamu* ya upendo WAKE kwa vidonda vya *makosa* ya mwanadamu. Leo, kupitia haya maono ya upendo, ya *Karatasi* ya MUNGU *Iliyoandikwa* na *Mkono*, tunakumbushwa hapa wazi wazi juu ya asili ya kilindini ya YEHOVA MUNGU *isiyochunguzika*. Katika mwaka huo, BWANA MUNGU wa Israel Alinituma Paris, Ufaransa kuwatangazia kwamba kurudi kwa Masihi sasa kumekaribia zaidi sana kuliko hapo mwanzo walipoamini. Kwa hivyo haya yamefanyika maono ya kushangaza zaidi ya yote katika nyakati zetu, kwa maana yalihusisha BWANA MUNGU MKUU MWENYEWE kunipokeza kihalisia Barua YAKE Binafsi Iliyoandikwa kwa Mkono. Mawasiliano ya moja kwa moja Jinsi hii ndio yaliyonishangaza sana; yaani jinsi MUNGU BABA anaweza kumkaribia mwanadamu kiasi hiki. Na basi umejitokeza kuwa mtembeleo ulio wa muhimu zaidi kanisani kwa sasa, katika mfululizo wa maono mengine makuu ambayo BWANA Amekuwa nayo pamoja na kanisa. Ni ya ajaabu kwamba haya Mazungumzo yote yasiyokoma yameelekezwa kwa siku inayongojewa sana kwa hamu na ghamu ya *unyakuzi*. Katika hiyo Mei tarehe 11 mwaka wa 2009, ilikuwa saa nane na dakika hamsini za usiku, nilipoyaona maono ya MUNGU MKUU yakifunuliwa moja kwa moja mbele ya macho yangu. Na ghafla bin vuu, katika hayo maono ya kipekee ya MUNGU, nilijikuta nikitembea kwenye njia nyembamba *iliyomulikwa* sawa sawa kutoka juu. Nilipoendelea kutembea ndipo niilipogundua kwamba ile nuru iliyokuwa *ikiangazia* ile njia nilioitembelea ilikuwa kwa kweli inatoka moja kwa moja mbinguni. Mung'ao wa mwangaza

ulioangaza kutoka juu mbinguni ulikuwa angavu sana kiasi ya kwamba ningeweza kihalisia kuuhisi uzito wa ile miale ilipong'aa kwenye njia. Pia Roho wa BWANA Alinisababisha nijue vyema ya kwamba hii ilikuwa *ardhi takatifu* zaidi kukutana nayo. Mwangaza wa ile *nuru* angavu ilioangaza kutoka juu, ndio ulioyoniwezesha kuona waziwazi kila mwamba na jiwe iliyokuwa kwenye ile njia niliyoitembelea usiku huo. Ama kweli, ni ule *mwangaza* angavu ulioniongoza salama katika njia hiyo pasipo kugonga hata moja wapo ya miamba iliyokuwa kwenye njia hiyo. Kisha kwa ghafla tena pasipo onyo lolote, Sauti kubwa ajabu ikanena kwa nguvu kutoka mbinguni ikisema,

"TAZAMA NA UKAONE NI NINI

KILICHOANGUKA MIGUUNI PAKO."

Yote ninayoweza kukumbuka bayana ni kwamba wakati BWANA Alinena katika hayo maono ya utukufu , badala ya kuitazama miguu yangu ili kujua kilichoiangukia, kutokana na mshtuko,mara moja nilitazama moja kwa moja juu yangu, na kuelekea angani ilikotoka Sauti kuu ajaabu ya BWANA. Sauti ya BWANA ilikuwa kubwa mno kiasi ya kwamba ilikuwa vigumu sana kwangu mimi kuipuuza katika hayo maono. Kwa hivyo, nilijaribu kutazama juu ambako MUNGU MKUU MWENYEZI Alikuwa Ameongelea. Ni wakati uo huo, nikiwa bado ninaangalia juu ili kujaribu kuona ni wapi sauti ilitoka, ndipo kwa kutokutarajia nilipata mshtuko mkubwa zaidi maishani mwangu nilipoona kile kilichoonekana kuwa *kipande* kidogo *cha karatasi* kikiwa kinaanguka kutoka mbinguni, na kuja moja kwa moja kunielekea. Kile *kipande cha Karatasi* nilichokiona kikiangushwa kutoka mbinguni, kilikuja moja kwa moja duniani na kikiwa kimenilenga mimi. Namna ile hicho *kipande cha karatasi* kiliachiliwa kutoka mbinguni, ilikisababisha kije kikielea hewani kama tiara. Nguvu za upepo zilipohimili uwezo wake wa kuelea, hiki *kipande cha karatasi* bado kiliendelea katika muanguko wake kuelekea dunia. Kile *kipande cha karatasi* nilichokiona kikielea huku kikija chini angani kutoka mbinguni, kilikuwa cha utukufu sana kiasi ya kwamba hata kiliangazia njia yake kuelekea duniani.

Wakati haya yote yalikuwa yakitendeka, mwangaza mkuu wa utukufu wa MUNGU kutoka mbinguni bado uliingazia njia yangu. Kile kilichonishangaza sana ni kwamba wakati nilipokawia kidogo kwa kuangalia ile njia chini ndipo nilishangaa kuona kwamba kile *kipande cha karatasi* kilichokuwa kikija kutoka mbinguni kilikuwa ghafla kimeanguka miguuni pangu. Ni lazima kilishika kasi isiyo ya kawaida kilipokuwa kikishuka ili kuweza kuanguka miguuni pangu ghafla. Ilikuwa imeanguka kwenye mguu wangu wa kulia.Katika maono hayo,nilipookota kile *kipande cha karatasi* cheupe na cha utukufu kilichokuwa kimeanguka tu kutoka juu, kwa haraka niligundua kwamba kwa kweli ilikuwa *Karatasi Iliyoandikwa* kutoka mbinguni. Huo ndio wakati ambapo hatimaye niling'amua uzito wa swala kwamba NILIKUWA TU NIMEPOKEA UJUMBE ULIOANDIKWA KUTOKA KWA MUNGU MKUU MWENYEZI ALIYE MBINGUNI. Huo ndio wakati nilipotambua kwamba MUNGU MKUU MWENYEZI MWENYEWE Alikuwa kwa hakika mara hii Ameamua kunitumia *Karatasi* halisi *Iliyoandikwa*. Kile kilichonishangaza hata zaidi,ni kwamba *Karatasi* niliyokuwa tu ndio nimeipokea,kwa hakika ilikuwa *Barua Iliyoandikwa* kwa *Mkono* na MUNGU wa mbinguni MWENYEWE. Ukweli wa mambo ulianza kufunguka hata zaidi nilipotambua kwamba kando na kuwa *Imeandikwa kwa Mkono*, Ile barua ya Kibinafsi niliyokuwa katika hatua ya kuipokea kutoka mbinguni katika maono haya, ilikuwa imeandikwa kutumia kalamu ya wino wa samawati. Katika maono haya ,nilipojaribu kusoma ile *Karatasi Iliyoandikwa kwa Mkono* niliyokuwa tu ndio nimeipokea kutoka mbinguni, hapo ndipo iliponishukia dhahiri kwamba maandishi ya hii barua ya kibinguni yalikuwa yametengenezwa katika mtindo wa kuteremka kuanzia juu hadi chini. *Kipande cha karatasi* kilichotumika kilikuwa cha utukufu wa kumetameta sana. Hiyo karatasi niliyoipokea ilikuwa imeandikwa mara tatu,katika njia ile ile na kwa kalamu ile ile ya wino.

Nilipoanza kusoma ile barua iliyoandikwa kutoka mbinguni katika mlazo wa daraja tatu, maandishi ya kwanza ya juu yalisoma;

***Ninakuja***

Nilipoendelea kusoma, maandishi ya pili katika mpangilio wa kushuka, yale yaliozingirwa katikati ya mawili, yalisoma;

***Ninakuja***

Na hatimaye, niliposoma fungu la tatu la hii *Barua* ya utukufu ya YEHOVA MUNGU wa Israel *Iliyoandikwa* kwa *Mkono*, Pia nayo ilisoma:

***Ninakuja***

Basi kwa ufupi, hivi ndivyo ujumbe wa MUNGU ulioandikwa kwa mkono kwenye *kipande cha karatasi* cha kimbinguni na cha utukufu ulivyosoma;

***Ninakuja***

***Ninakuja***

***Ninakuja***

Nilipoamka kutoka katika maono hayo ndipo nilipoitazama saa na kutambua kuwa ilikuwa yapata saa Nane na dakika hamsini za usiku. Pia nikaanza kwa polepole kukumbatia ukweli wa kustaajabisha na wa kugutusha ya kwamba BWANA MUNGU MKUU ALIKUWA tu Amenitumia *Barua Iliyoandikwa kwa Mkono.* MUNGU WA MBINGUNI Alikuwa tu Ameniandikia kama rafiki anavyo mwandikia rafiki. Hiyo ilikuwa ya kushangaza sana! Hata hivyo ujumbe kwa kanisa uko dhahiri sana kwa kuwa unasema kuwa BWANA Anakuja. Lakini kwa BWANA kuisema mara tatu kuwa Masihi Anakuja, bila shaka inaashiria kwamba kwa kweli, mara hii, ANAKUJA. BWANA Analiambia kanisa kwamba linahitajika *kujiandaa* katika *uhaki* na *utakatifu kamilifu* ili kuweza kumpokea Masihi Ajaye.Pia inaashiria swala kwamba wakati umekwisha.▪

CONGO, BRAZZAVILLE / JULAI 2014





MASIKIO KIZIWI KABISA YAZIBUKA NA KUFUNGUKA/ Alikuwa kiziwi tangu kuzaliwa lakini BWAN Akayafungua masikio yake kiziwi.